

## 3 Yohana

*Salamu*

<sup>1</sup> Mzee:

Kwa Gayo rafiki yangu, nimpendaye katika kweli.

*Gayo Anasifiwa Kwa Ajili Ya Ukarimu Wake*

<sup>2</sup> Mpendwa, naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya njema kama vile roho yako ifanikiwavyo.

<sup>3</sup> Ilinifurahisha sana baadhi ya ndugu walipokuja na kutueleza juu ya uaminifu wako katika kweli na jinsi unavyoendelea kuenenda katika hiyo kweli.

<sup>4</sup> Sina furaha kubwa kuliko hii, kusikia kwamba watoto wangu wanaenenda katika kweli.

<sup>5</sup> Rafiki mpendwa, wewe ni mwaminifu kwa yale unayowatendea ndugu, ingawa wao ni wageni kwako.

<sup>6</sup> Wameshuhudia kuhusu upendo wako mbele ya kanisa. Utafanya vyema ukiwasafirisha kama inavyostahili kwa Mungu.

<sup>7</sup> Ilikuwa ni kwa ajili ya hilo Jina waliondoka, bila kukubali kupokea msaada wowote kutoka kwa watu wasioamini.

<sup>8</sup> Kwa hiyo imetupasa sisi kuonyesha ukarimu kwa watu kama hao ili tuweze kutenda kazi pamoja kwa ajili ya kweli.

*Deotrefe*

<sup>9</sup> Nililiandikia kanisa, lakini Deotrefe, yeye apendaye kujifanya wa kwanza, hakubali mam-laka yetu.

<sup>10</sup> Hivyo kama nikija, nitakumbuka matendo yake atendayo, akitusingizia kwa maneno ya hila. Wala hatosheki na hayo anayotusingizia, bali pia hukataa kuwakaribisha ndugu, na hata huwazuia wale walio tayari kufanya hivyo na kuwafukuza watoke kanisani.

### *Demetrio*

<sup>11</sup> Rafiki mpendwa, usiige lile lililo bayo bali lile lililo jema. Yeyote atendaye mema atoka kwa Mungu, bali atendaye mabaya hajamwona Mungu.

<sup>12</sup> Kila mtu ameshuhudia mema kuhusu Demetrio, vivyo hivyo hata na hiyo kweli yenyewe. Sisi pia twashuhudia mema juu yake, nanyi mwajua kwamba ushuhuda wetu ni kweli.

### *Salamu Za Mwisho*

<sup>13</sup> Ninayo mambo mengi ya kukuandikia, lakini sipendi kuandika kwa kalamu na wino.

<sup>14</sup> Badala yake, nataraji kukuona upesi, nasi tutaongea pamoja ana kwa ana.

<sup>15</sup> Amani iwe kwako. Rafiki zetu walioko hapa wanakusalimu. Wasalimu hao rafiki zetu walioko huko, kila mmoja kwa jina lake.

**Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™  
Swahili: Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia  
Takatifu™ (Bible)**

copyright © 2018 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili

Translation by: Biblica, Inc.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2021-04-12

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 18 Apr 2025 from source files dated 31 Aug 2023

9cbb05be-39f3-5d18-8b2a-4ba788541462